# Ile Mbegu Haitarithi Pamoja na Kapi

Asante sana, Ndugu Demos. Na sasa tuna furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, na kusikia shuhuda hizi nzuri kutoka kwa watu hawa wazuri, na sasa tunatumaini ya kwamba Mungu ataendelea kuwa pamoja nasi na kutubariki.

2 Sasa, usiku wa leo, nasikia ya kwamba napaswa kuzungumza usiku wa leo, Bwana akipenda. Na nilimwuliza Ndugu Shakarian, muda mchache tu uliopita, nilisema, "Sasa, usione aibu. Ninajua inatubidi kutoka hapa saa tano nami—nami ninashindwa kuchunga wakati ninapokuja hapa."

3 Inaonekana kama sisi wengine wote hufanya hivyo. Tunajisikia . . . Wanasema, "Dakika mbili, dakika tatu, ama . . . " Ndugu Smith, unajua, hilo ni gumu kulifanya katika dakika mbili ama dakika tatu. Nami ninajua jinsi ilivyo, na ninamsikitikia kila mmoja. Bali tuko kwenye wakati wa majira, mahali tulipo. Tunaelekea kwenye Umilele, lakini sasa tuko kwenye wakati.

4 Nami nilisema, "Ndugu Demos, kidogo tu kabla ya wakati, usione aibu, nivute tu kwenye koti langu nami nitajua ya kwamba ni wakati wa kuondoka." Sasa, kama simalizi, nitamalizia usiku wa leo. Kwa hiyo kama nikifanya hivyo, vema, nina somo jipya kwa ajili ya usiku huu.

5 Sasa kabla tu hatujafungua Kitabu, hebu na tuzungumze na Mwandishi wake, huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

6 Baba mpenzi wa Mbinguni, tunakushukuru asubuhi hii kwa ajili ya kusanyiko hili, kwa yale ambayo tumekwisha sikia. Kama tu ungetujaza na baraka sasa, Bwana, tungejisikia ya kwamba ilikuwa ni vema kuwa hapa. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba Wewe utaendelea, kama ni sawa machoni Pako, na uendelee kuwa pamoja nasi na kutusaidia. Na sasa tunakusanyika kwenye Neno. Kama vile tulivyojikusanya kwenye ushirika wa sisi kwa sisi, tukisikia ushuhuda wa vile ulivyotufanyia, sasa jalia turudi katika Neno na tuone mahali ambako haya yote yanatoka. Ndipo, hilo litakuwa ni thibitisho la yale tunayosikia na kuona, yakitukia leo. Tujalie mambo haya katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

7 Sasa, kama—kama mtumishi Wake, ni—ninawajibika kwa Ujumbe. Na mara nyingi nimeeleweka vibaya sana, katika nyakati zilizopita, na labda daima nitaeleweka vibaya. Lakini sisemi mambo mara nyingine nipate kuwa—kuwa tofauti, ninayasema nipate kuwa mwaminifu. Nami ninapenda kusema

yale ninayofikiri ni sawa. Kila mtu ana—ana haki ya mambo hayo, kutoa maoni yake mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu mimi niko miongoni mwenu.

8 Na Ndugu Shakarian, akizungumza kuhusu kadi za maombi katika mistari ya maombi, kwa kuona yale Roho Mtakatifu . . . Sasa, hakusema jambo hilo kunihusu mimi. Hayo ni kuhusu Roho Mtaktifu, kwa maana nisingeweza kufanya mambo hayo. Kila mtu anajua, ya kwamba nisingeweza kuyafanya. Lakini—lakini hilo ni jambo dogo, unaloona hapa. Laiti mngalikuwako kule kwingine, muone vile anavyotabiri mambo! Na mimi . . . mambo yatakayotendeka, ni, haya ni ninii tu . . . ninyi, ninyi ndio mnaofanya hayo. Ninyi ndio mnaomwamini Mungu.

9 Na—na sasa kama humwamini Mungu, kumbuka, Yeye anakwambia jambo hilo, papa hapa jukwaani. Na kama uko dhambini, Yeye anakwambia. Na mambo ambayo umefanya na hukupaswa kufanya, Yeye anakwambia. Si yale tu wanayoweka kwenye kadi ya maombi. Wangeweza kuandika kwenye kadi yao ya maombi . . . Wasingesema, kwenye kadi hiyo, walikuwa ni wenye "dhambi," na mwanamke huyu alikuwa "anaishi na mume asiye wake," ama vitu kama hivyo. Nao hawatayaandika hayo kwenye kadi ya maombi, bali Roho Mtakatifu anachomoa hilo hata hivyo, unaona. Unaona? Na kwa hiyo basi liko sasa (vipi) katika sehemu ya ki—kiroho, enyi marafiki.

10 Nami ninasema jambo hili kwa uaminifu. Maana, hatuko wengi hapa asubuhi ya leo, ni kundi dogo tu. Linanishangaza sana, mpaka linanifanya kuwa na wasiwasi sana, mara nyingine ninajisikia tu kama kutaka kupiga mayowe. Na wakati ninapoketi chini mahali fulani, kando ya mlima, ambako ninatumia wakati mwingi sana kule, nikipokea kutoka kwa Mungu, ninashuka na kuwapa watu yale Yeye aliyonipa. Nami—nami sitaki kwenda kinyume na watu. Lakini hata hivyo, kuwa mkweli, yanibidi niwe mwaminifu kwa Mungu, unaona, kwa—kwa Ujumbe.

11 Na sasa sisi, Bwana akipenda, tunajitayarisha kuondoka mara moja kwa ziara ya nchi za ng'ambo, katika siku chache tu, na kama hayo ni mapenzi ya Bwana. Hakika ninayadhamini maombi yenu.

12 Mnaonekana mmejaa furaha! Ninapoanza kuzungumza, ninasahau wakati kabisa, kama na vile ilivyo na wengine wetu. Lakini kwa Ndugu Shakarian, hawa wahudumu wazuri hapa jukwaani, na huko nje, ninyi nyote mlio marafiki wa Yesu Kristo, ninawasalimu katika Jina Lake; kama—kama ndugu mwenzenu pamoja nanyi, kwa msalaba, kwa Mungu, tukiwa ndugu na dada.

13 Ninataka kufungua, asubuhi ya leo, katika Maandiko, katika Kitabu cha Wagalatia, Bwana akipenda. Ningependa kusoma Andiko fulani.

14 Sasa, jana usiku, niliposikia ujumbe uliotolewa na ndugu yetu muhudumu hapa jukwaani, yeye alinena kwa lugha. Bredesen, Ndugu Bredesen, mtu mzuri sana. Mimi . . .

15 Kuona jambo hili kwa ukosefu wangu wa kisomo na elimu, kutoelewa kwangu kwa maneno, na halafu nikijua Ujumbe huu ni kweli, na kuona mtu kama huyo aliyekuwa kwenye ile paneli hivi majuzi usiku, akisimama pale, na ambaye anaweza kukabiliana na wale wenye elimu. Huenda wao wasiweze kufanya yale ambayo Bwana ameniitia kufanya. Mimi siwezi kufanya yale ambayo Bwana amewaitia kufanya. Bali sisi tukifanya kazi pamoja., nina hakika tunaweza kuupeleka Ujumbe kule, kama tu tukikaa mbele za Mungu.

16 Na wakati alipotoa u—ushuhuda hapa jana usiku. Naye Roho Mtakatifu akanena kwa lugha, na, mtu fulani huko kwa wasikilizaji, sikuzote ninajua kuheshimu jambo hilo. Maana, ninafahamu, kwa Biblia, huyo ni Roho wa Mungu akituletea jambo fulani. Naye alisema, alinena juu ya mvua ya vuli, mvua ya masika na mvua ya vuli. Na hilo linanileta kwenye wazo fulani.

17 Ya kwamba Ndugu Bonham alikuwa ndiyo tu kwanza anipe kifurushi kidogo chenye hundi ndani yake, kasema, “Hili ni toleo la upendo kwa ajili ya . . . kutoka kwa watu.” Sasa, yeye—yeye, hawakupaswa kufanya hivyo. Unaona, mimi sikuja hapa kwa kusudi hilo. Lakini mimi . . . yeye, walinitolea mimi, na, bila shaka, kungekuwa na . . . hakuna njia ya kuzirudisha. Nami nitazichukua, Bwana akipenda, na kujaribu kuziweka kwenye matumizi yangu, kwenda nchi za ng’ambo. Kwa sababu, mimi sasa hivi sidhaminiwi, kwa njia yo yote, kule ninakoenda.

18 Kwa namna fulani ni siri, kwa kuwa makanisa hayataniruhusu niingie. Nami ninaenda huko kama mwindaji, kwa maana ni kwa ajili ya Bwana wangu. Bwana ameliweka moyoni mwangu kufanya jambo hilo, nami sina budi kuingia kwa namna fulani ya kujifanya. Unaona? Kwa hiyo wana mawazo madogo ya kuchekesha kule, ya kwamba kila mmoja wao anataka nitie sahihi kadi fulani, ya kwamba nitakubaliana nao juu ya yale wanayoamini, na niseme eti kundi *hili* lingine limekosea, na kundi *hili* linasema wataniingiza kama nitasema kundi *hili* liko makosani.” Unaona? Lakini mimi sipendi jambo hilo. Unaona, tuna . . .

19 Daima nimejaribu kusimama katikati ya watu, nje ya madhehebu na tofauti zao, na kuita kile kilichoonekana kama Roho wa Mungu alikuwa akisema kupitia kwa ndugu hapa asubuhi ya leo, ya kwamba sisi si madhehebu. Sisi ni watoto wa familia fulani. Sasa, hakuna madhehebu ya Branham. Kuna familia ya Branham, nasi sote hatujiungi na familia hiyo, tunazaliwa katika familia hiyo. Na kwa hiyo, mimi, hilo ndilo ninalojaribu kuwakilisha, vi—vizuri nijuavyo.

20 Sasa katika Wagalatia 4:27-31, ninaamini nimeyaandika hapa chini, ningetaka kusoma hili kwa ajili ya somo.

> *Kwa maana imeandikwa, Furahi, wewe uliye tasa, usiyezaa; paza sauti, ulie, wewe usiye na utungu; maana watoto wake aliyeachwa pekee wana-. . .ni wengi kuliko wa huyo aliye na mume.*
>
> *Basi, ndugu zangu, kama ilivyokuwa Isaka sisi tu watoto wa ahadi.*
>
> *Lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyomwudhi yule aliyezaliwa kwa Roho, ndivyo ilivyo na sasa.*
>
> *Lakini lasemaje andiko? Mfukuze mjakazi na mwanawe, kwa maana mwana wa mjakazi hatarithi kabisa pamoja na mwana wa mwungwana.*
>
> *Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana.*

Bwana na aongeze baraka Zake sasa kwenye Neno Lake la thamani.

21 Nina machache, jana usiku niliandika mambo machache; na ilikuwa kwamba, wakati nilipokuwa na mkutano mmoja tu kwa juma, mahali fulani, ni—niliweza kukumbuka Maandiko hayo dhahiri sana akilini mwangu. Lakini sasa baada ya mimi . . . Sasa, kama ninavyosema kwa mzaha kidogo, simaanishi kufanya mzaha hapa kwenye jukwaa hili. Lakini baada ya kupita umri wa miaka ishirini na mitano, mara ya pili, sikumbuki kama nilivyokuwa nikikumbuka. Kuna ninii nyingi sana . . . Ford hii ya kale imesafiri maili nyingi, na kwa hiyo sikumbuki. Lakini mradi tu ninaweza kusogea, ninataka kutoa kila hatua kwa utukufu wa Yeye aliyeniokoa.

22 Sasa mimi, nikiwaona basi asubuhi ya leo, nikiwaangalia . . . Labda hili linaonekana ni la kushangaza, na labda kwa mtu anayetumia akili huenda likaonekana lote ni jambo la mchanganyiko, bali linakubaliana na jambo nililoitiwa. Hata kila kitu kidogo ni ishara kwangu. Ninakiangalia, ninaona jinsi kinavyotenda kazi. Hivyo ndivyo ninavyopata ujumbe wangu mara nyingi, na ni kuangalia na kuona jinsi Roho anavyotenda kazi, na kuona jinsi *huyu* anasema nini, *yule* anasema nini.

23 Na mmeniona mimi, mara nyingi, kabla ya ibada ya kuponya, nimesimama hapo jukwaani, ama nimeketi kitako, nikiangalia. Ninamhisi Roho, jinsi anavyotembea, na tayari ninajua mtu huyo anayeketi pale ana shida gani. Unaona? Ninaliona kule, hapa *hivi*, unaona, unalikamata jambo hilo hata kabla hujaenda jukwaani.

24 Mara nyingine kabla sijaja mkutanoni, mara nyingine, kabla hata ya kuja hapa kama vile California, nimeketi chini na wale walio pamoja nami, nikasema, “Kutakuwako na jambo fulani

litakalotukia, *hili* litatukia hapa, na *hili* litatukia chini hapa, litaenda *hivi*," unaona, kwa maana liko katika Roho wa Mungu. Yeye ndiye ninii... Yeye alijua mambo yote tangu mwanzo, unaona, na kwa hiyo Yeye ndiye wa Milele.

25 Halafu kuona, asubuhi ya leo, Ndugu Jewel Rose, rafiki na ndugu yetu sisi sote wa thamani sana, jinsi ambavyo aliamka na kusoma Zaburi hiyo. Angalia jinsi hilo lilivyounganika, kama vile yeye alivyosema, "Ninataka kuona ni mbegu ya aina gani inayoning'inia juu yako." Jana usiku, Roho alinena akasema, na kuhusu, "Mvua ya vuli, mvua ya masika na ya vuli, zote mbili zikinyesha katika siku za mwisho." Na asubuhi ya leo, "Mbegu inayoning'inia juu yako." Unaona, Roho akizungumza, angalia jinsi alivyofanya kupitia kwa wahudumu hawa, na kadhalika, asubuhi ya leo. Kwa hiyo basi ninachukua somo hili: *Ile Mbegu Haitarithi Pamoja na Kapi*.

26 Hilo ni somo la kushangaza sana, bali, *Ile Mbegu Haitarithi Pamoja na Kapi*. Na kutoka katika kuchukua, nikitoa maamuzi yangu juu ya jambo hili, ama somo langu, hasa, kutoka katika Wagalatia 4:27, tatu, Paulo hapa bila shaka anazungumzia juu ya mzao halisi wa wana wawili wa Ibrahimu. Sasa, hili, ninataka kutumia hili ili kwamba mwe na hakika hamtalikosa. Na kama nikipitisha wakati, nitalichukua tena usiku wa leo. Nami ninataka kufundisha, kama tu somo la shule ya Jumapili, ili kwamba mpate kuninii, ninaamini, mtapata kulifahamu vyema zaidi.

27 Sasa, na baadhi yenu ninyi wanaume ambao mna—mna uwezo zaidi wa kufanya jambo hili kuliko mimi ninavyoweza kulifanya, mbona... mimi si mwanatheolojia, kwa vyo vyote vile. Na kwa hiyo kama msipokubaliana na mimi juu ya jambo Hili, jisikieni tu kama vile nilivyojisikia jana usiku wakati dada fulani mpendwa hapa waliponipikia sambusa ya cheri. Nikiketi kwenye ninii ya—yangu... kwenye chumba changu cha hoteli asubuhi ya leo, ni—niliuma mbegu, bali bado ningali ninakula sambusa. Niliondoa tu hiyo mbegu, mnaona. Kwa hiyo, hiyo ni, yale usiyoamini juu ya jambo Hilo, yaweke tu kando, unaona, na wewe uendelee tu kula kile unachofikiri ni cha kweli.

28 Sasa, Paulo anazungumzia juu ya wana wawili wa Ibrahimu, ambao, mmoja wao alizaliwa na Sara na huyo mwingine na Hajiri. Sasa tunaona hapa ya kwamba, na tunafahamu jambo hilo kupitia kwenye Maandiko, ya kwamba Mungu kamwe hawakilishwi na mbili. Ni katika tatu. Daima ni katika tatu, ndipo Mungu anapokamilika.

29 Hisabati za Biblia zina utaratibu kamili. Mungu hukamilika katika tatu, anaabudiwa katika saba, na kadhalika. Unaona, kwa hiyo tu—tunaona ya kuwa hisabati ya Biblia hazikosei hata kidogo.

30 Nasi hapa tuna wana wawili wa Ibrahimu, na hata hivyo tunaweza tu kuwa warithi mradi tu sisi tu mmoja wa hao wana, ama mwana fulani wa Ibrahimu. "Kwa maana sisi tukiwa wafu katika Kristo, basi tunakuwa uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi pamoja Naye kulingana na ahadi," kwa hiyo inambidi Ibrahimu kuwa na Mwana mwingine.

31 Sasa, tunajua ya kwamba mwanawe wa kwanza alizaliwa na Hajiri, na tunaona ya kwamba mwanawe wa pili alizaliwa na—alizaliwa na Sara. Bali yeye alikuwa na Mwana wa tatu, ambaye alikuwa ni Yesu. Sasa, hilo linaweza likaonekana ni geni, bali hilo ndilo tutakalojaribu kulielezea. Kama nilivyosema, Mungu hujiwakilisha Mwenyewe, daima katika ukamilifu, katika tatu. Nami nimejiweka wazi mbele za watu wote sasa, na zaidi sana kwenu wanatheolo-. . .wanatheolojia, kwamba mambo haya yako tu jinsi ninavyoliona, jinsi linavyonijia mimi.

32 Kama vile hapo mwanzo, Mungu, Mungu aliishi peke yake, kwa maana Yeye alikuwa ni wa Milele, unaona, hata hakuwa ni Mungu. *Mungu* ni "kitu cha kuabudiwa." Na ile Logos, kama tunavyoiita, lile Neno lililotoka kutoka kwa Mungu, Kwamba, kila mtu anajua ya kwamba Huyo alikuwa ni Malaika wa Bwana, ama Neno la Bwana, lililowafuata Israeli jangwani; Malaika wa Agano, Logos iliyotoka kwa Mungu. Ndipo huyo Logos alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Sasa tuko katika Yohana Mtakatifu mlango wa 1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Na sasa, wakati alipoutoa uhai Wake kwa ajili yetu, ndipo Roho Wake anarudi juu yetu. Yesu alisema, "Katika siku hiyo mtajua ya kwamba mimi niko ndani ya Baba Yangu, Baba ndani Yangu; Mimi ndani neyu, nanyi ndani Yangu."

33 Unaona, ni Mungu, daima, Mungu akijidhihirisha Mwenyewe, akitenda kazi kupitia katika nyakati mbalimbali. Kwa hiyo hizo tatu, za, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule akifanya kazi katika sifa tatu. Na sisi leo tu mmoja, Kanisa Lenyewe, sifa za mawazo ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuwa na Ka—Kanisa. Kwa hiyo wale waliokuwa katika Kristo walikuwa katika Kristo hapo mwanzo, hao walikuwa ni mawazo Yake, na mawazo Yake ndiyo sifa Zake.

34 Hapa ndipo uzao unapoanza, katika ile ahadi. Na Ibrahimu hapa kidogo alitilia shaka, kwa Ishmaeli. Nami ninataka kuwaonyesha zile hatua tatu za hizi, za Mzao huu ambao tutauzungumzia habari zake, ambao hautarithi pamoja na kapi. Sasa tunaona ya kwamba, katika mwanzo hapa, ya kwamba Mungu alimpa Ibrahimu ahadi.

35 Alimpa Adamu ahadi, kwanza. Na hiyo ilikuwa, ama, ile ahadi ilikuwa ina masharti. "Kama hutafanya jambo *hili*. Kama utafanya jambo *Hili*."

36 Lakini wakati alipompa Ibrahimu hiyo, halikuwa na masharti, "Nimelifanya jambo hilo tayari." Yeye kamwe... Alichofanya, kilikuwa hakina masharti, alimpa Ibrahimu. Sasa, na kupitia hiyo, Ibrahimu akiwa na ahadi, kwa hiyo inatubidi kuwa Mzao wa Ibrahimu. "Haikuwa tu ni kwa Ibrahimu, bali kwa Mzao wake baada yake." Sasa kama utaangalia, haikuwa "wazao" baada yake, bali "Mzao" baada yake.

37 Sasa tunaona ya kwamba ile ahadi, kwa kutiliwa shaka kidogo na Sara, ndipo Sara alimwambia Ibrahimu amchukue huyu Hajiri, yule Mmisri, kijana mwanamke, awe mkewe, na hivyo ndivyo Mungu angemuinua huyu mzao wa ahadi.

38 Sasa, unaona, kutokana na yale niliyosema jana usiku, hatua yo yote kutoka kwenye hilo Neno la asili la Mungu inavuruga mambo yote. Hatuwezi kuondoka kutoka kwenye hilo Neno la asili. Inapaswa...Tulizungumza juu ya jambo hilo jana jioni, ama hivi majuzi jioni, hasa, juu ya Balaamu. Yeye alipata jibu la Mungu, la moja kwa moja na dhahiri, "Usiende!" Lakini yeye ana mapenzi ya kuruhusia. Na unaweza kufanya kazi katika hayo ukitaka, na Mungu ataheshimu jambo hilo, lakini bado si mapenzi makamilfu ya Mungu. Na hayo ndiyo tunayopaswa kushindania, mapenzi Yake makamilifu, si mapenzi Yake ya kuruhusia. Ufalme wa Mungu, ambao Yeye...uko duniani leo, utaninii...kamwe hauwezi kuanzishwa, kwa haki, juu ya mapenzi ya kuruhusia. Inabidi kurudi kwenye mapenzi Yake makamilfu.

39 Sasa tunaona hapa ya kwamba Sara, baada ya Mungu kumwambia Ibrahimu ya kwamba huyo mtoto angezaliwa kupitia kwa Sara, ambaye angebariki ulimwengu, sasa Sara alitilia shaka jambo hilo. Nami ninataka mwone, halikupitia kwa Ibrahimu; bali kwa Sara, mwanamke. Naye alilitilia shaka, akasema, "Mchukue Hajiri." Naye Ibrahimu hakutaka kufanya hivyo, bali Mungu akamwambia aende zake akafanye hivyo haidhuru. Kwa hiyo akamwoa, akitilia shaka kidogo. Sasa, Isaka, akiwa ndiye huru na anayetoka kwa mwanamke wa ahadi, asingerithi pamoja na Ishimaeli, mjakazi, katika shaka.

40 Hayo ndivyo Paulo aliyokuwa akijaribu kusema hapa. Unaona, ambapo jambo moja linatiliwa shaka, na linaangusha jambo fulani la Mungu, utaratibu fulani wa Mungu, bali hautarithi pamoja na utaratibu wa asili wa Mungu. Mnaelewa? Unaona, hauwezi kurithi.

41 Sasa hiyo ndiyo sababu ninasisitiza sana leo. Nami nilifikiri huu utakuwa ni wakati mwafaka, kwa maana sijui tutakuwa pamoja kwa muda gani zaidi, na, labda ningeweza, kwa namna fulani Mungu angenisaidia kuwaonyesha sababu inayonifanya nishutumu madhehebu ya kidini kwa uthabiti sana. Unaona? Unaona, hayawezi kurithi pamoja na mpango wa asili wa Mungu, kwa maana madhehebu si ya Mungu.

Ni ya mwanadamu. Kanisa la kwanza lililopata kufanywa madhehebu, katika dunia nzima, lilikuwa ni kanisa Katoliki la Kirumi huko Nikea, Urumi. Ufunuo 17, ilisema, "Alikuwa ni kahaba, na watoto wake wote walikuwa ni malaya." Na kahaba ni mwanamke asiyeishi mwaminifu kwa mumewe, na malaya ni kitu kile kile. Lakini, unaona, lilikuja kuwa kanisa, hata hivyo. Ni mfumo wa kimadhehebu na unatenga undugu. Tulijaribu kuunganisha makanisa yote pamoja. Halitafanikiwa; Hilo hailijapata kufanikiwa. Halitafanikiwa (kamwe). Baraza la Makanisa Ulimwenguni, wao wananinii tu. . . wao wako nje ya mpango wa Mungu.

42 Sasa mnasema, "Wewe ni nani, jamaa unayesimama pale hapo bila hata elimu ya shule ya sekondari?" Hilo halileti tofauti yo yote, ni elimu gani. Si elimu yangu ninayojaribu kuzungumzia.

43 Ni Neno la Mungu ninalozungumzia, unaona. Na shuhuda hizi unazoona katika huduma hii, si mimi, ni Mungu akijaribu kuwafikishieni jambo hilo, ya kwamba ni Kweli. Je! Mungu angekuwa na uhusiano wo wote na uongo? Basi isiwe kwangu, kumtumikia Mungu ambaye angebariki uongo. Yeye hubariki Kweli, ile Kweli ambayo Yeye aliheshimu.

44 Sasa, Ishmaeli hangeweza kurithi pamoja na Isaka, kwa maana mmoja alitiliwa shaka kidogo, alitiliwa shaka kidogo tu. Alikuwa ni mtoto, ailikuwa angali ni mzao wa Ibrahimu, bali si njia kamilifu ya Mungu ya jambo hilo; Ishmaeli. Sasa ningeweza kutumia wakati mwingi hapa, bali ninatumaini Roho Mtakatifu atawafahamisha jambo hili katika njia halisi ipaswayo. Sasa kama wao. . .

45 Kama Ishmaeli na Isaka wasingeweza kuwa warithi pamoja kwa maana mpango wa asili wa Mungu ulibadilishwa ukawa m— mpango wa kuruhusia wa Mungu, mpango wa kuruhusia ambao Mungu alibariki, wala Kanisa la Kiroho leo haliwezi kurithi pamoja na la kimadhehebu. Madhehebu, Mungu aliyabariki, kama alivyombariki Ishmaeli, bali wa Kiroho hawatarithi pamoja na hao wengine. Hiyo ni kweli. Kutakuwako, kutoka katika kanisa la kimadhehebu (linalojiita kanisa, kanisa la kawaida) atatokea Bibi-arusi wa Kristo, Mteule.

46 Sasa hapo, kile kinachonisumbua katika saa hii, ni kujua ya kwamba tunaona madhehebu haya yote yakijiingiza katika kitu hiki ambacho tunajua kuwa ni. . . kile mnachoita mvua ya vuli, ama, kumwagwa kwa Roho. Je! mnatambua ya kwamba Yesu alisema, ya kwamba, "Hapo hilo litakapotukia, itakuwa ni wakati wa mwisho"? Wakati, yule mwanamwali mjinga na mwanamwali mwenye busara, hawakuwa warithi pamoja. Kwa kuwa wakati. . . Yule mwanamwali mjinga, yeye alikuwa ni bikira, alikosa tu Mafuta. Lakini wakati alipokuja kununua Mafuta, ilikuwa ndio wakati ambapo Bwana Arusi alikuja. Naye

akaachwa, wakati akijaribu kununua Mafuta. Je! mnaelewa hilo? Ninataka hilo lizame ndani, vizuri sana. Sasa, hakika haitanilazimu kuendeleza somo hilo mbali zaidi. Sasa, wala wa Kiroho na wa kawaida hawawezi kuwa warithi pamoja.

47 Hiyo ndiyo sababu Kunyakuliwa, Bibi-arusi, mwanamwali mwenye busara, yule aliyeitwa atoke, aliyechaguliwa tangu zamani, aliyeteuliwa! Mbona, ninyi wafanyi biashara hamngeendesha ofisi zenu kama vile watu wengine wanavyojaribu kufikiri ya kwamba Mungu huendesha mpango Wake, ovyo ovyo. Mungu alijua, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa. Kwa kuchagua tangu zamani, kwa kujua tangu zamani, Yeye aliona kila mshiriki, akaweka kila jina kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, kabla hata Kanisa halijaanza kwanza. Yesu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyekuwa kwenye Kitabu hicho. Yeye alinunua Kitabu cha Ukombozi. Kilikuwa kimepotea, Naye akatukomboa, na majina yote yaliyokuwa katika Kitabu hicho yalikombolewa hapo Yeye alipotukomboa.

48 Halafu, kama vile nilivyosema mara nyingi, unatambua jambo hilo. Hiyo ndiyo sababu uko hapa asubuhi ya leo, ndiyo sababu mnatoka katika madhehebu haya yote na kadhalika. Ninyi ni ninii. . .Kuna kitu fulani kinachowavuta. Kama vile wazo langu dogo lilivyokuwa, kuhusu yule tai aliyeanguliwa chini ya kuku, unaona, u—unatambua kuna jambo fulani la tofauti. Ka—kanisa halikuwa na kitu fu—fulani kinachoridhisha. Lakini, wewe, ulisikia kitu kingine kilichokuwa ni mlio, ulitambua ya kwamba, ya kwamba ulizaliwa kwa ajili ya jambo Hilo. Wewe ni sehemu Yake. Wewe, unaenea katika Hilo, kama glavu mkononi. Na hiyo ndiyo sababu tumekusanyika pamoja hapa asubuhi ya leo, ni kwa sababu, kama vile mama yangu wa kusini alivyozoea kusema, "Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba," kwa maana mna ushirikiano.

49 Mwewe na hua hawana ushirikiano. Mlo wao ni tofauti, ingawa hua angeweza kuanguliwa chini ya mwewe. Hiyo ni kweli. Inategemea ilikuwa ni nini, kwanza. Sasa, na katika jambo hilo, ingawaje, hu—hua huenda ikambidi kulelewa kwa muda kidogo na huyo, na huyo mwewe, bali hatimaye atampata mwenzi wake.

50 Hivyo ndivyo kanisa linavyofanya siku hizi, kwa kuwa Yesu ni Neno Naye ni Bwana Arusi, na Bibi-arusi ni sehemu ya Bwana Arusi. Kwa hiyo Neno ambalo itapaswa litimizwe siku hii ni sehemu ile ile ya Neno lililotimizwa katika siku Zake, na ni Neno lile lile, tukio lile lile, Maisha yale yale.

51 Kwa maana, wakati Mungu alipomtenganisha Adamu, yeye alikuwa ni vyote viwili. Tunaona kwamba, Adamu alikuwa ni roho, kwanza. "Alimfanya mtu katika mfano Wake Mwenyewe, alimwumba mwanamume na mwanamke." Na halafu, Mwanzo 2

na kuendelea, Alimumba mtu katika . . . kutoka katika mavumbi ya ardhi. Mtu aliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mungu ni Roho), kwa hiyo yeye ni mtu-roho. Basi alipofanyika mtu mwenye mwili, mwili wa mnyama duniani, Yeye ana-—Yeye anaonyesha, anamwonyesha hapa Bibi-arusi. Yeye hakuchukua na kuumba kiumbe kingine, bali alichukua sehemu ya Adamu, ule uumbaji asili, akatoa kwake, ubavu kutoka ubavuni mwake; kisha akatoa roho ya kike kutoka kwa Adamu, akaacha roho ya kiume mle ndani, na akaiweka katika sehemu ya kike. Kwa hiyo, sehemu ya roho yake, sehemu ya mwili wake; mwili wa mwili wake, mfupa wa mfupa wake; Neno la Neno Lake, Uzima wa Uzima Wake, na hivyo ndivyo Bibi-arusi alivyo kwa Kristo!

52 Hiyo ndiyo sababu Kunyakuliwa kwa Mzao wa kifalme hakuna budi kuja kwanza. Na hao wafu waliosalia hawakuishi tena kwa muda wa miaka elfu moja, kisha wakaletwa kwenye ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi. Unaona, hakuna hukumu kwa Mzao wa kifalme, ama Mzao aliyechaguliwa tangu zamani wa Ibrahimu. Sasa kama utachukua Yohana Mtakatifu 5:24, sikiliza jambo hili, "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele."

53 Sasa hilo lingekuwa tofauti jinsi gani na theolojia zetu chungu zima? Sasa ningeweza kutoka hapa na kumwambia mlevi, "Je! unaamini?" "Hakika!" Mtu aliye na mke wa mtu mwingine, "Je! unaamini?" "Hakika!" "Je! uliketi mkutanoni jana usiku, kusikiliza Neno?" "Hakika!" "Unaliamini?" "Hakika!" Anasema tu jambo hilo.

54 Lakini fasiri ya asili ya Neno hili, ni "yeye *anayelifahamu* Neno Langu, na atamwamini Yeye aliyenipeleka." "Yeye anayelifahamu," yaani, yeye anayefahamishwa hilo.

55 Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watakuja. Kondoo wangu, hua Wangu, huisikia Sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata." Na Sauti ya Mungu ni nini? Ni Neno la Mungu. Sauti ya mtu ye yote ni nini ila ni neno lake? Ni Neno la Mungu; watalisikia Neno la Mungu.

56 Ile mbegu ya kawaida basi ilikuwa ni mbebaji, kupitia kwa Ishmaeli kwanza, pili Isaka, halafu na kuendelea tu hata kwa ule Mzao. Ni kama vile tu shina, kishada, na kapi, vya mhindi. Sasa, hapa, zile hatua tatu za mbegu zinatuonyesha picha ya kweli ambayo ninawataka mwiangalie pamoja nami asubuhi ya leo. Tunaona hapa.

57 Na kwa kutokuwa na elimu, inanibidi kuchukua mambo ya kawaida ninayoona, kuonyesha mambo ya kiroho ninayofunuliwa, kwa maana nisingeweza kuyaelezea kwenu vizuri kwa ufasaha wo wote wa maneno.

58 Na, hata hivyo, Mungu daima huwakilisha mambo ya kiroho kwa mambo ya kawaida. Kama Biblia isingalikuwako, bado

ningejua ya kwamba Ukristo ulikuwa ni sahihi, kwa kuwa dunia yote huenda katika mzunguko wa kufa, kuzikwa, na kufufuka. Maumbile yanatenda kazi katika kufa, kuzikwa, na kufufuka.

59 Angalia utomvu kutoka kwenye mti, jinsi unavyoleta jani, na tunda, linaanguka; otomvu unarundi ardhini kwa sababu ya majira ya kipupwe, huko chini ndani ya udongo; unarudi tena katika majira ya kuchipua, ukiwa na uhai mpya. Kila mwaka, ukishuhudia ya kwamba kuna kuishi, kuna kufa, kuna kufufuka.

60 Jua huchomoza asubuhi, mtoto mchanga ndiyo kwanza azaliwe, mnyonge sana. Saa moja au saa mbili, linaanza kwenda shuleni. Saa nne ama tano, limemaliza shule. Linanaangaza kwa nguvu zake zote, kutoka kama kwenye saa tano mpaka saa tisa, kisha linaanza kudhoofika. Jioni linashuka, linakuwa dhaifu, ni mzee. Je! huo ndio mwisho wake, linakufa? La. Linachomoza tena kesho yake asubuhi. Unaona?

61 Maumbile yote, Biblia yako halisi na ya kweli ambayo inashuhudia pamoja na Biblia hii! Na hilo ndilo ninalojaribu kuwaonyesha sasa asubuhi ya leo, kupitia kwenye maumbile utaona Neno la Mungu, yakifananishwa na—na Neno la Mungu, kwa maana maumbile yamefanywa na Mungu.

62 Kama vile sayansi, wanapata mbinu za mitambo na kanuni za maumbile, bali hawajui maumbile hayo ni kitu gani. Hawajui Uhai wa maumbile. Huo ni Mungu. Kwa hiyo, mitambo pasipo elimumwendo haifai kitu.

63 Sasa, shina, kishada, na kapi, angalia. Hajiri hapa aliwakilisha shina, ambalo lilikuwa ni uhai wa kwanza ulioanza katika ahadi. Sara anawakilisha kishada, ama chavua, inayotokea kwenye kishada. Mariamu, yule bikira, aliwakilisha na kuzaa ule Mzao wa kweli wa kiroho, apate kuleta shina halisi na la kweli. Hajiri na Sara, wote wawili walikuwa kwa njia ya kujuana kimwili. Lakini Mariamu, yule bikira, alikuwa ni kwa nguvu za Neno la Mungu lililoahidiwa, kwa kuzaa kibikira. Alizaa ule Mzao halisi. Lile shina, Hajiri, mke wa pili, kwa shaka ya ahadi, ikitenda kazi kwa kutilia shaka, kidogo.

64 Ninatumaini tu, Mungu na atusaidie. Mimi sininii... Ninawatakeni mwone jambo hili, vibaya sana. Huwezi kutilia shaka sehemu yo yote ya Hilo. Inakupasa kulichukua tu jinsi lilivyo. Halihitaji kufasiriwa ko kote. Biblia inasema ya kwamba, "Neno la Mungu si la kufasiriwa apendavyo mtu ye yote." Mungu hahitaji ya shule zo zote zetu kulifasiri Neno Lake. Wakati Yeye anapolithibitisha na kulifanya hai, hiyo ndiyo tafsiri Yake. Wakati Mungu aliposema, "Na iwe nuru," kukawa na nuru. Hilo halihitaji kufasiriwa. Wakati aliposema, "Bikira atachkua mimba," alichukua mimba. Halihitaji kufasiriwa.

65 Hatuhitaji haya yote, maseminari na kadhalika ndizo zinazowashika watu, "Vema, *sisi* tunayo fasiri yake. *Sisi* tuna fasiri yake."

66 Mungu Mwenyewe hufasiri Neno Lake. Yeye hahitaji mtu mwingine ye yote kumfasiria. Alisema, "Litatukia," na linatukia. Alisema, "Katika siku za mwisho, Yeye angemwaga Roho Wake," alimmwaga. Sijali madhehebu yalisema nini. Yeye alitenda hilo, hata hivyo, maana alisema angetenda. Kwa hiyo, halihitaji kufasiriwa, kwa maana Mungu hujifasiria Mwenyewe.

67 Na mambo haya unayoona, ambayo yanaonekana ni mageni kwako sasa. Kama mkiweza, hebu kumbukeni; huduma yenu, ninyi Wapentekoste, huko nyuma miaka thelathini ama arobaini iliyopita, ilikuwa ni jambo geni kabisa kwa—kwa kanisa la Kimethodisti na la Kibatisti, kama vile Hili lilivyo kwenu leo. Lakini sasa hebu lipate Hiyo kwenye Neno. Ninajaribu kuwaonyesha kama vile mlivyojaribu kuwaonyesha wao. Na basi kama Mungu akigeuka na kusema Hilo ndivyo lilivyo, katika Neno, kisha analithibitisha kwamba ni la kweli, hiyo ndiyo fasiri ya Mungu Mwenywe. Huhitaji mtu ye yote akufasirie.

68 Sasa, Hajiri, kwa kuninii "kidogo"! Kumbuka, hauwezi kutoa Neno moja kutoka Humo. Na Yesu alisema, katika Ufunuo, mwishoni mwa Kitabu hicho. Na mwanzoni mwa kitabu, Kristo alisema, "Mtu ye yote aliyetoondoa Sehemu moja kutoka kwenye Neno hilo!" Neno moja tu kufasiriwa vibaya, lilisababisha kila ugonjwa, kifo, tulichowahi kuwa nacho. Vema, kama Mungu, ambaye ni mtakatifu, aliangalia chini; na kusababisha mchafuko huu wote kwa kufasiri tu Neno moja vibaya, na jambo lo lote dogo dhidi ya Neno hilo kuu lilisababisha machafuko yote haya; na mateso, kutokwa na damu na kufa kwa Mwanawe wa Pekee, kupatanisha jambo hili baya sana Kwake; tutaingiaje pasipo kutimiza Neno lote?

69 "Vema," ulisema, "Ndugu Branham, hiyo ilikuwa katika Mwanzo." Nilihisi jambo hilo, unaona.

70 Lakini hebu nikwambie, Ufunuo, hiyo ni sehemu ya mwisho ya kile Kitabu. "Mtu awaye yote atakayeondoa Neno moja kutoka katika Kitabu cha unabii huu, au kuongeza neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa kutoka katika kile Kitabu cha Uzima."

71 Yesu alisema, katikati ya Kitabu hiki! Hao hapo mashahidi wako watatu tena: Mwanzo, Agano Jipya, na siku hii ya leo. Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

"Vema, Yeye hakumaanisha jambo hilo."

72 Yeye alikuwa akizungumza na watu waliokuwa ni wanatheolojia, wa hali ya juu sana. Wale makuhani, babu wa babu wa babu wa babu wa babu zao ilibidi wawe ni makuhani.

Kulichukulia vibaya Neno moja Lake, mbona, ilikuwa kabisa ni hukumu ya kifo. Ilibidi wapigwe mawe, Neno moja likiondolewa. Bali walikuwa na fasiri mbaya Yake. Kwa hiyo wakati Neno Lenyewe; wakati Mungu alipoahidi kumtuma Masihi, na akamtuma katika nguo zile zile za kitoto alizoahidi kwamba angekuja nazo, wao walikuwa na nguo nyingine za kitoto za kumvika.

73 Hebu niseme jambo hili. Ndivyo ilivyo siku hizi, kwamba wao hawalipati Hilo! Haliko katika nguo za kitoto za umadhehebu ama za kiakili. Liko katika nguo za kitoto za nguvu na ufufuo, na madhihirisho ya Kristo aliyefufuka, vile Mungu alivyoahidi Hilo, wala si katika nguo za kitoto za mawazo ya watu juu ya jambo Hilo.

74 Sasa, Hajiri, kwa tofauti moja ndogo, kupitia kwa mwanamke, si kwa kupitia kwa Ibrahimu sasa. Ibrahimu hakutaka kufanya jambo hilo, bali Mungu alimwacha alifanye kwa sababu yeye. . .Jinsi ile ile, alivyomwacha Balaamu kuendelea. Sasa angalia, kwa kutokukubaliana Nalo kidogo, yeye alimzaa Ishmaeli, ambaye alikuwa ni punda-mwitu, hawezi kamwe kutiishwa. Aliishi kwa uta wake. Alikuwa ni punda-mwitu. Angali ni punda-mwitu, siku hizi.

75 Sasa Sara, kile kishada, ama chavua, Sara, yule mke wa kweli wa ile ahadi, anamzaa mwungwana, hatimaye likazaliwa taifa lililoahidiwa.

76 Sasa, bali, Mariamu, bila kujuana kimwili, bali kwa ahadi, kama tu vile Ibrahimu alivyopata ile ahadi kutoka kwa Mungu, Neno la Mungu, bali aliamini ile ahadi, "Tazama mjakazi wa Bwana," unaona, akaleta si shina, bali Mzao wa asili, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno ambalo Ibrahimu aliamini na ambalo Mariamu aliamini.

77 Sasa, Mariamu hakuwa ule Mzao, yeye alikuwa ni kapi tu kupitia kwa ule Mzao. Hao wengine wawili walikuwa ni wabebaji wa uhai, ni mzao tu wa asili. Mariamu hakuwa ule Mzao, yeye mwenyewe; lakini kama vile ilivyo imani katika Neno la Mungu, alizaa sura halisi zaidi ya Neno, kwa maana yeye alikuwa ni Neno. Lakini kama vile kapi lilivyo, ile ninii. . .ya ngano, punje ya ngano, kapi hushikilia ngano ndani yake na kuilinda mpaka inapoweza ama imekomaa hata inaweza kujitegemea. Unaona? Ndipo, Mzao Mwenyewe ndiye aliyemwacha. Kama vile tu, ule Mzao ulikuwa tumboni mwake, yeye hakuwa ule Mzao. Hakuzaa ule Mzao. Mungu ndiye ile Mbegu.

78 Sasa, ile damu basi, watu wengi wanafikiri ya kwamba tuliokolewa kwa damu ya Kiyahudi. Na baadhi yao walisema, "Vema, tuna haki kupitia kwa Mataifa, kwa kuwa yule kahaba Rahabu na—na Ruthu yule Mmoabu, na kadhalika, walikuwa ni

Mataifa." Huna dai la jambo hilo hata kidogo, hata mmoja wao. Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa.

79 Alikuwa ni Mungu, yule Logos, lile Neno lililotoka kwa Mungu. Wakati, alipoanza kuatamia juu ya dunia, na akaleta viumbe vya baharini. Wakati Roho wa Mungu, yule Logos, lile Neno, ambalo Mungu alisema, "Iwe," ndipo hapo Logos akatokea, ambaye ni Neno. Ndipo Neno likaanza kuninii . . . maana yote haya yalikuwa ndani ya Logos; Neno lote la Mungu, Biblia nzima, kwa kila wakati. Basi Logos alipoanza kupulizia juu ya nchi, kukatokea viumbe vya baharini; kisha ikaendelea kujengeka, uhai wa ndege, ikaendelea hata kufikia uhai wa mnyama. Na hatimaye kukatokea kitu fulani kiwakilishi, ama kilichoonekana kama kile kitu kilichokuwa kikikitengeneza, kikikiatamia, Mungu, mtu katika sura kamili ya Mungu.

80 Mtu huyo akaanguka, kama vile mbegu ambavyo haina budi kuanguka. Na ndipo Mungu akaanza kuatamia juu ya hiyo, baada ya kule kuanguka. Akamtoa He—Henoko, akamtoa Eliya, akamtoa Musa, akamtoa nabii baada ya nabii, akijaribu kuirudisha sura hiyo tena. Na, hatimaye, usoni pa nchi kukatokea sura halisi ya Mungu Mwenyewe tena, ambayo ilikuwa ni Mungu, yule Logos aliyefanyika mwili akakaa kwetu.

81 Sasa Logos yeye yule ana sehemu, Yeye ana Bibi-arusi, na Logos yeye yule, Neno hili ambalo haliwezi kubadilishwa, linaatamia juu ya makanisa siku hizi, likifanya bidii kurudisha Neno katika dhihirisho Lake kamili. Ambapo, ma—manabii walikuwa ni wabebaji wa Mbegu hiyo, na makanisa ya kimadhehebu yamekuwa wabebaji wa hiyo Mbegu sasa. Sasa angalia, upesi, bali kama vile kapi linavyokumbatia, linavyoshikilia ile Mbegu basi, kisha linaiachilia.

82 Yesu alikuwa ni Mungu. Yeye alikuwa ni Mungu. Baba Yake alikuwa ni yule Logos Mkuu Mwenyewe. Naye asingeweza kuimwaga Hiyo yote katika Musa, kwa maana yeye alikuwa ni nabii.

83 Nalo Neno la Bwana daima, halikosei kamwe, humjia nabii. Hakuna mahali, hakuna wakati, katika Biblia, ama tangu Biblia, ambapo fasiri sahihi ya Neno iliwahi kumjia mwanatheolojia. Haliko katika Maandiko. Si kwa Mafarisayo, wala kwa Masdukayo, na wala Mungu kamwe hajamwinua nabii kutoka miongoni mwa mojawapo wa hao, na wala Yeye hakufanya hivyo katika siku hizi za mwisho.

84 Mara wanapolileta, wote hukusanyika pamoja na kuunda madhehebu kwalo, papo hapo linakufa. Bali kuna kusudi la Yeye kufanya jambo hili. Tutajaribu kueleza jambo hilo, Mungu akitusaidia. Hebu angalia, angalia hapa jinsi mwanamke, kanisa, ile mbegu sasa, inavyoaza kuonekana kama ile Mbegu Yenyewe.

85 Sasa unaona, wakati mbegu inapoingia ardhini, ni mbegu halisi. Wakati inapochipuka, inaleta uhai. Lakini uhai unafanya nini inapopasua kutoka kwenye mbegu ya ngano? Hauzai shina lile lile la ngano papo hapo, ama punje ile ile ya ngano. Ni uhai wa ngano, bali uko katika hatua ya mbebaji. Na hayo yalikuwa ndio yale matengenezo ya kwanza, wakati Luther alipojitokeza kutoka katika lile giza la machafuko. Ilibidi ife.

86 Mara nyingi sana, watu husikitikia. Loo, nami nilisoma kitabu si muda mrefu uliopita, juu ya, *Mungu Mkimya*, kilichotolewa na baadhi ya hawa wanafalsafa wa kisasa wanaojaribu kukuondoa kwa Mungu. Kama hujui Neno la Mungu na mpango wa Mungu, unaweza kutikiswa kwa urahisi. Bali unapoona mpango wa Mungu, utaratibu Wake, basi kwa imani unajua ni Mungu; na Mungu akijitambulisha mwenyewe, akifanya yale tu aliyofanya katika—katika nyakati nyingine, akitembea, akithibitisha.

87 Hiyo ndiyo sababu Musa asingeweza kutikisika. Alizungumza uso kwa uso na Mungu, na Mungu akamwambia, "Mimi ndimi niliyekuwa na Ibrahimu kule nyuma. Mimi ndimi niliyetoa ahadi hii. Nitakuwa pamoja nawe." Utawezaje kumzuia mtu huyo basi?

88 Kama vile yule nabii wa kale alivyosema, "Simba akinguruma, ni nani asiyeweza kuogopa? Na Mungu amenena, ni nani asiyeweza kutabiri?" Wakati tunapoona mambo ambayo Mungu aliahidi katika saa hii, kuona yakitukia, unawezaje kunyamaza unapoona ya kwamba hiyo ndiyo njia Yake? Kile alichosema, kingetukia. Unaona mambo hayo yote ya siri, lakini hivyo ndivyo hasa Mungu alivyosema hayo yangetukia.

89 Sasa angalia, "mwanamke," yule mbebaji. Sasa, Hajiri alitokea kama shina, ndipo chavua ikatokea, na halafu kapi linatokea, na ndipo Mbegu ikaja. Sasa angalia wabebaji hawa, ninataka uangalie, kwanza.

90 Sasa, shina halifanani hata kidogo na Mbegu, bali Uhai uliokuwamo katika Mbegu umo kwenye shina. Huyo alikuwa ni Luther. Sasa, shina hilo dogo lina majani mengi; yalitoka kwa Luther, yakaingia kwa Zwingli, na kuendelea mpaka kwa Calvin na wengine wengi.

91 Sasa angalia, basi, iliondoka hapo ilipokuwa. Angalia maumbile sasa yakifuata mpango wa Neno la Mungu, kama vile jua; kufa, kuzikwa, na kufufuka. Ndipo ikaja chavua, huyo alikuwa ni Wesley. Na kupitia hupo kulikuwa na chavua nyingi ndogo zikining'inia kwake, ambazo kwa kweli zilifanana zaidi na ile Mbegu kuliko vile hilo jani lilivyofanya, kwenye hiyo ngano ama mahindi. Ilifanana sana nayo; kwa sababu, Wesley akiwa na Neno la pili, Neno la pili la Mungu, akilileta kanisa Lake, alipitia katika utakaso. Huo ndio uliokuwa ujumbe wake. Vema.

92 Basi, baada ya kitambo kidogo, huo ukaondoka ndipo ukaingia kwenye shina tena, na kuzaa suke la mahindi. Lakini kabla suke hili halijaanza, kulikuwako na kuvi, kapi, kifuniko, ganda. Na mkulima ye yote wa ngano, mkulima wa mahindi, kama ukifumua mle ndani na kutoa hilo suke la mhindi ama hilo suke la ngano, utafikiri ya kwamba hicho kininii kidogo—hicho kidude kidogo cha kwanza ndicho hiyo punje ya ngano. Lakini, sasa, huo hapo wakati wa Kipentekoste. Sasa huwezi, wewe, mwanatheolojia ye yote ama . . .

93 Mwana historia ye yote, hasa, anajua ya kwamba hizo ndio zile nyakati, jinsi zilivyokuja. Chukua Ki—Kitabu cha Ufunuo, chukua nyakati za kanisa, uone kama hivyo sivyo hasa zinavyojitokeza.

94 Sasa, kutoka kwa Wesley kukaja Pilgrim Holiness, Wanazarayo, na hayo makanisa yote madogo ya utakatifu, walio karibu sana na Neno kuliko vile matengenezo ya Kilutheri yalivyokuwa. Bali, unaona, wakati Luther alipounda madhehebu, hilo lilianzisha tu yale majani. Na wakati hili lilipotukia, wote wenye Roho wakaondoka kwenye kanisa la Kilutheri, wote ila tu wale wa kimadhehebu, na wale waamini halisi na wa kweli wakaingia katika utakaso.

95 Na kisha wakati utakaso ulipopiga hatua, Wapilgrim Holiness, na kadhalika, na madhehebu yote ya utakatifu, Wanazarayo, na kadhalika, waliondoka huko, wakaingia moja kwa moja katika wakati huu wa Kipentekoste. Basi angalia hiyo chembe ndogo sasa, ya ngano, inaonekana mara milioni moja zaidi kama ile ngano ya asili, iliyoingia ardhini, kuliko lile shina lilivyokuwa ama vile chavua ilivyokuwa. Lakini kama utaketi chini, uiweke chini ya darubini, na ufungue maskini makapi hayo madogo, hayo pia ni mabebaji tu. Ile punje haijaanza bado. Ni chipukizi dogo sana kule ndani kabisa, ukiwa na darubini kubwa yenye nguvu unaweza kuona ncha hiyo ndogo, kama ncha ya pini, hiyo hapo mbegu inakuja. Na kapi hili hapa linalofanana kabisa na kitu chenyewe, sio kitu chenyewe. Ni tumbo la uzazi tu.

96 Ni kama vile tumbo la uzazi la Mariamu. Mariamu hakuwa ile Mbegu, katika uwakilisho hapa wa shina. Yeye alikuwa tu ni mbebaji Wake, kama hao wengine. Lakini kwa kuwa aliitwa na kuchaguliwa kwanza, na Mungu Mwenyewe, kwa kusudi hili, ilionekana zaidi sana kama vile marafiki zetu Wakatoliki wangewazia, ya kwamba yeye alikuwa ni mama wa Mungu. La, yeye hakuwa mama wa Mungu, wala hakuwa Mbegu ya Mungu.

97 Mwanamke hutoa yai. Mungu anatoa u—uhai. Hemoglobini, damu, iko katika jinsia ya mwanamume.

98 Kuku anaweza kutaga yai ama ndege anaweza kutaga yai, katika majira ya kuchipua ajenge kiota chake, lakini, kama ndege huyo wa kike hajashiriki na ndege wa kiume,

halitaanguliwa. Limekufa. Litaozea moja kwa moja katika kiota.

99 Kama ninavyosema mara nyingi, hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi, yanaozea moja kwa moja kwenye kiota, kinachoitwa Methodisti, Baptisti, Pentekoste, na kadhalika. Kama hawana uhusiano na Neno, Lenyewe, wataozea moja kwa moja katika kiota, katika madhehebu yao.

100 Sasa, sasa baadhi yao husema basi, Waprotestanti kwa namna fulani huamini ya kwamba Mariamu ndiye aliyetoa lile yai. Kama hivyo ndivyo ilivyo, angalia kile unachomfanya Yehova Mungu kufanya. Hilo yai haliwezi kutolewa bila hisia fulani.

101 Kwa hiyo, unaona, Mungu alifanya yai na seli zazi pia, aliumba vyote viwili katika tumbo la uzazi la Mariamu. Na Mtu huyo hakuwa kitu cho chote ila ni Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili na kukaa kwetu, Imanueli, si mtu mzuri tu, nabii; Yeye alikuwa Mtu mzuri na Nabii; si mwalimu, mwanatheolojia. Loo, huenda—huenda alikuwa hayo yote; alikuwa yote katika yote. Lakini zaidi ya hayo yote, alikuwa ni Mungu Mwenywe. Biblia ilisema, "Tumeokolewa na Damu ya Mungu." Mungu Mwenyewe, si nafsi ya tatu ama nafsi ya pili. Yule Mtu, Mungu Mwenyewe, Yehova mkuu, alimtia Mariamu uvuli; na Muumba, na akaumba hiyo seli ya damu, ule uhai, na pia lile yai.

102 Kama unaweza kumfanya Myahudi kuona jambo hilo, wewe, yeye anajua Masihi ni nani. Wakati yule John Ryan alipoponywa kule Benton Harbor, alikuwa kipofu kwa muda wa miaka arobaini. Huyo rabi aliniuliza, akasema, nilikuwa na mahaojiano naye, alisema, "Huwezi kumkata Mungu katika vipande vitatu na kumpa Myahudi."

103 Nikasema, "Wengine wao hufanya hivyo. Lakini sisi hatumkati Mungu katika vipande vitatu." Nikasema, "Je! unaamini manabii?"

"Bila shaka, ninaamini manabii," akasema.

104 Nikasema, "Je! Isaya alinena habari za nani, Isaya 9:6, 'kwa ajili yetu mtoto amezaliwa'?"

Akasema, "Mbona, ilikuwa ni Masihi."

105 Nikasema, "Masihi atakuwa na uhusiano gani na Mungu?" Hilo lilitosha. Nikasema sasa . . .

Akasema, "Yeye atakuwa ni Mungu."

106 Nikasema, "Kweli kabisa. 'Ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.'"

107 Hapo ndipo wa umoja walipokosea, hapo ndipo wa utatu walipokosea, pande zote mbili za barabara. Bali wastani wa kufaa ni papo hapo katikati. Kama Mungu angaliweza kuwa

Baba Yake Mwenywe, kama Yesu angalikuwa ni Baba Yake Mwenyewe, asingeweza kuwa. Na kama alikuwa na Baba mwingine mbali naMungu, na Biblia ilisema "Roho Mtakatifu" alikuwa ndiye Baba Yake, na kama hao ni roho mbili mbali mbali, Yeye alikuwa ni mtoto haramu. Hiyo ni kweli. Ni nani aliyekuwa Baba Yake, Mungu ama Roho Mtakatifu? Sema mmoja na utaona jinsi utakavyoaibika. Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

108 Mathayo 1:18, Yeye alisema.

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.*

109 Sasa Baba Yake ni Nani? Unaona, unaona ninalomaanisha? Angalia

> *. . . Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri,* kwa njia hii.
>
> Angalia*, basi alipokuwa akifikiri hayo, . . . malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua katika* nanii wako*. . . Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza* wa . . . [Kusanyiko linasema, "*. . . Roho Mtakatifu*"—Mh.]

110 Nilidhani wao walisema, "Mungu Baba alikuwa ndiye Baba Yake"? Loo, enyi wanatheolojia, ufahamu wenu uko wapi?

Angalia, "Kutakuwako Nuru wakati wa jioni!"

111 Mzao wa kweli ulikuja kupitia kwa Mariamu, bali haukuwa ni Mbegu yake. Ilikuwa ni ahadi ya Mungu, ambapo alisema, "Tazama mimi ni mjakazi wa Bwana." Wabebaji wa uhai walikuwa ni wanawake. Na sasa, Mariamu, Mzao huo ulifanana zaidi sana.

112 Ilimbidi Hajiri kulipokea kwa njia iliyopotoshwa. Sarah, akitilia shaka kitu hicho, aliifikisha tu kwenye mbegu ya kawaida, tamaa ya kujuana kimwili. Lakini Mariamu, bila kujuana kimwili ko kote, aliamini Neno, nalo Neno llifanyika mwili.

113 Lakini angalia, Mariamu akiwa karibu sana, alishikilia Mbegu hiyo tumboni mwake, na ilionekana kana kwamba ingekuwa ni Mbegu yake. Na ndivyo ilivyo kwa Wapentekoste. Nitakuja nyumbani. Lakini kumbuka, Yesu alisema, katika Mathayo mlango wa 24, kifungu cha 24 "Katika siku za mwisho, hizo roho mbili . . . " Si katika siku za mwanzoni, sasa. "Katika siku za baadaye, hizo roho mbili zingefanana sana hata ingewapoteza walio wateule kama yamkini." Roho ya

Kipentekoste, kama tu kitu halisi kabisa, kikamilifu sana hata ingewapoteza walio wateule kama yamkini.

114 Sasa, hayo si maneno yangu. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Sasa, baada ya kitambo kidogo, labda mtapata ufahamu wa yale ninayojaribu kusema. Sasa Mbegu hiyo bila shaka ilifanana sana . . .

115 Hilo kapi lilifanana sana na ile Mbegu, hata zaidi ya vile chavua ilivyokuwa, na zaidi ya vile shina lilivyokuwa, lakini hizo zilikuwa tu ni bebaji za ile Mbegu. Unaona, Luther aliunda madhehebu, hilo shina likafa; Wesley aliunda madhehebu, hiyo chavua ikafa; Pentekoste iliunda maehehebu, huo uhai ukafa. Ndipo sasa inakuja ile Mbegu. Huwezi kuendelea mbele zaidi ya Mbegu.

116 Angalia, katika miaka yote huko nyuma, wakati huduma kubwa inapoinuka, upesi sana madhehebu yanaifuata. Ufufuo hudumu miaka mitatu hivi, ndipo wanaufanya kuwa madhehebu, wanaunda madhehebu fulani. Inabidi yatokee mengi kutoka kwake; kama vile mengi yalivyotoka kutoka kwa Luther, yale majani; na mengi kutoka kwa chavua, Wesley; na majani ya Kipentekoste yakitokeza, umoja, uwili, utatu, unne, utano. Loo, rehema! Unaona?

117 Lakini, angalia, miaka ishirini ya kudhihirishwa kwa Yesu Kristo! Hakuna hata madhehebu moja yameinuka, na hakuna hata moja yatakayoinuka; yatakufa kama vile kila moja la ufufo wa mvua ya vuli, na mengine yote. Huu ni wakati wa mwisho, ile Mbegu, wala haitarithi pamoja na kapi, si zaidi ya vile Ishmaeli alivyokuwa mrithi pamoja na Isaka.

118 Unaona hapa sasa jinsi lilivyo karibu, liko karibu vya kutosha kuweza kupoteza. Luther, lile shina; Wesley, kile kishada; na Mariamu, lile kapi, ama tumbo la uzazi, ama Pentekoste. Jinsi ningeweza kuendelea papa hapa kuhusu lile kapi, na kuwaonyesha. Katika nyakati zote huko nyuma, halijafanana sana kama ilivyo sasa. Kila kitu ni *kanisa*, lile kanisa, unaona, yule "mwanamke."

119 Pia angalia, ilikuwa ni "mwanamke," hapo mwanzo, ambaye alishuku ile ahadi ya kwanza. Si kwamba Mungu alighairi Neno Lake. Mungu haghairi Neno Lake leo; Yeye anathibitisha Neno lake la asili! Lakini Sara alisema, "Labda, huenda ikawa; tunangojea."

120 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, unajaribu kukwea uingie katika kitu ambapo hujui unachokwea. Utafanyaje jambo hilo usipokuwa unajua unachofanya? Je! unatembea ukiwa umefungwa kitambaa usoni? Ukijaribu kupanda uingie katika kitu ambapo hujui unachofanya, utaanguka. "Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, wote wawili wataanguka shimoni," Yesu alitoa matamshi hayo.

121 Bali sasa tunasimama kwenye wakati wa ile Mbegu. Sasa Mbegu itashikilia, (nini?) itasaidia, itashirikiana na ile Mbegu ikiishikilia. Iliwekwa hapo kwa kusudi hilo, kuishikilia.

122 Kwa sababu, wakati jua linapochomoza mwanzoni mwa msimu wa kuchipua, juu ya ngano, angalia maumbile yote yakipitia katika msimu, yakipita katika siku, kila kitu kinapita kikamilifu kabisa, pamoja na Mungu. Sasa wakati hilo jua lenye joto linapoanza kuangazia ile mbegu, inatokeza. Lakini nchi inapaswa kuwa katika hali fulani kuifanya hiyo Mbegu ichipuke kutoka kwenye udongo. Inapaswa kuja namna hii, na kufikia hali fulani kuifanya hiyo mbegu ichipuke. Inapaswa kuja namna hiyo, ipate kuitoa kutoka kwenye . . . kutoka kwenye wakati wa giza.

123 Watu fulani, huyu mkosoaji niliyesema aliandika kile kitabu, *Mungu Mkimya*, yeye alisema, "Kote katika zile nyakati za giza, maskini hao wafia imani walikufa, waliangamizwa, hao Wakristo, na Mungu ameketi Mbinguni kama kwamba hata hakuhusika." Mbona, maskini mtu huyo mjinga, kipofu, kipofu wa kiroho, laiti macho yake yangalifunguliwa! Hivi hujui mbegu inapaswa kukaa ardhini, ipate kufa na kuoza, kabla haijazaa tena?

124 Na kanisa la kipentekoste lilikufa, kupitia Katoliki la mwanzoni. Na lilitokea tu katika mfano wa shina, lakini unaona jinsi linavyoumbika vizuri, kila moja kupitia kwenye wakati wa Lutheri, Wesley, Kipentekoste? Mnafahamu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

125 Sasa halina budi kurudi moja kwa moja kwenye huduma hiyo ya asili aliyokuwa nayo hapa duniani, maana ni Bibi-arusi. Wao ni mmoja. Sasa, Yeye aliahidi, katika siku za mwisho, jinsi mambo haya yangetukia. Na tunayaona yakitukia, kama ilivyo zile ahadi zote, Malaki 4, Luka Mt. 17:30. Loo, ni Maandiko mangapi zaidi, yasingekuwa na mwisho!

126 Na, loo, itanibidi kusimama, maana tumechelewa. Naam. Vema, u—unaambia, angalia kama wanaweza kupata . . . Waulize, unaona, na ndipo uje uniambie. Sasa, hebu kdiogo. Ninataka sana kulifikia jambo hili, sana. Ni—ninataka mwone jambo hili, sana. Angalia, Yesu . . . Angalia, unaona, Bibi-arusi.

127 Hata hivyo, tunaona, katika wakati huu tunaoishi sasa, unaona, ya kwamba lile tumbo la uzazi, yale madhehebu ya Kipentekoste, yalifanana kabisa na kile kitu chenyewe. Lakini je! ulitambua ya kwamba, Ufunuo 17, uliliita kanisa Katoliki la Kirumi, yale madhehebu ya kwanza, "kahaba"? Ni wangapi wanaojua jambo hilo ni kweli? Ni wangapi wanaojua alikuwa ni mama wa makahaba? Mwanamke mzinzi ni kitu gani? Sasa, Yeye alisema mwanamke huyu alikuwa ni lile "kanisa." Kahaba ni kitu gani? Ni mwanamke asiye mwaminifu kwa nadhiri yake ya ndoa. Malaya ni kitu gani? Jambo lile lile, neno lile lile.

128 Sasa, yeye alizaa. Ni uzazi wa namna gani? Si kwa Neno, bali uzazi wa kimadhehebu. Hawa hapa Methodisti, Baptisi, na Wapentekoste, nao wote walichukua tabia za mama yao. Mwanamke awaye yote mkaidi hapa California anaweza kumzaa msichana bikira; na hiyo ndiyo sababu ujumbe wa kwanza ulitokea, lakini wakati kweli ilipowakilishwa wakati wa Luther, ya utakaso, yeye asingeweza kuipokea. Wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu uliporuhusiwa, ulipopewa Wamethodisti, wasingeweza kuupokea. Na sasa wakati ambapo wakati wa Mbegu umezaa mpentekoste, hawezi kuupokea. Ameunda madhehebu. Bali amekuwa mbebaji wa ile Mbegu, unaona.

129 [Ndugu fulani anane kwa lugha. Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Amina. Sasa Bwana na ashukuriwe kwa ajili ya jambo hilo, Neno, urahisi wa Neno lililosemwa.

130 Unaona, ni rahisi tu, kama tu katika jambo hili, ni kama tu kuangalia mahidi yakikua. Huhitajii kuwa na tafsiri kubwa ya kitheolojia fulani ya jambo hilo. Wewe yaangalie tu. Wewe ni ninii . . . Yeye yuko moja kwa moja karibu nawe, sikuzote. Unaona, ile . . . ni ninii . . .

131 Sina budi kufunga. Nimesikia mtu akinivuta, nami nilimwomba afanye hivyo. Hatuna budi kufunga. Sasa, ndugu, nitatoa tamshi moja tu, ndipo nitaondoka.

132 Angalia, sasa. Lile kapi, shina, na kadhalika, ni wabebaji tu wa Neno. Wao walikuwa na sehemu ya Neno, unaona, mpaka walipofikia kwenye; kuhesabiwa haki, kutakaswa, kurudishwa kwa vipawa katika—katika Wapentekoste. Lakini sasa angalia. Kama tu ilivyokuwa kwa Ishmaeli, Isaka, unaona, na halafu kwa Yesu; unaona, mmoja alikuwa amepotoshwa, mwingine alikuwa wa asili, na hii hapa ile Mbegu Yenyewe inakuja. Unaona? Sasa, kanisa limekuja kutoka katika kitu hicho hicho, likarudi moja kwa moja. Kama vile ua ama cho chote kile, linakunywa maji, linaingiza, na kuenda . . .

133 Hiyo haina maana ya kwamba Walutheri wamepotea. Walutheri walioukataa utakaso, wangepotea, ambao wanataka kushikilia kwenye kitu fulani . . . Unaona, Israeli walikuwa mana mpya kila usiku, unaona. Angalia.

134 Lakini sasa katika wakati wa mwisho, angalia kapi hili hapa, sasa angalia, katika ngano. Siri yote ya—ya uhai imetiwa muhuri ndani ya hilo kapi. Tunaina lo katika Luther, ikija. Tunaiona katika kishada, ikitoka. Tunaiona katika shina. Tunakuja hapa, na sasa imefikia kwenye umbo la kapi, karibu sana na vile ilivyokuwa kwenye ule wakati wa kipentekoste, lakini siri halisi imefichwa ndani.

135 Sasa kumbukeni, kulingana na Ufunuo, siri yote ya kile Kitabu imetiwa muhuri kwa Mihuri Saba, ambapo wale watengenezaji hawakupata nafasi ya kuileta, zile hatua nne za matengenezo, zile hatua nne za Wenye Uhai wanne waliotoka

wakaenda kukabiliana na zile nguvu nne za ulimwengu. Wa kwanza aliyetoka, alikuwa ni . . .

136 Wa kwanza aliyetoka akaenda alikuwa ni nani? Simba, kukabiliana na wakati wa Kirumi. Huyo alikuwa ni Neno, lile la asili. Yeye ni Simba wa kabila la Yuda. Kristo Mwenyewe alitoka akaenda kukabiliana na wakati huo. Mnyama wa pili alikuwa ni nani aliyetoka akaenda kukabiliana; mnyama wa pili aliyetoka akaenda, kukabiliana na yule mpanda farasi mwingine, yeye alikuwa ni nani? Unaona, yule mpanda farasi wa kwanza alikuwa amevaa mavazi meupe, ametiwa taji kichwani mwake, baadaye, kadhalika, bali uta usio na mishale.

137 Angalia farasi wa pili aliyetoka akaenda, yule Mwenye Uhai aliyeenda kukabiliana naye alikuwa ni ndama. Ndama ni mnyama wa dhabihu. Waliangamizwa katika ufia imani kwenye ule wakati wa giza.

138 Mwenye Uhai wa tatu aliyetoka akaenda kukabiliana na farasi aliyefuata, kabla ya yule farasi wa mauti kutokea, mauti na kuzimu, farasi aliyefuata . . . Mwenye Uhai mwingine aliyeenda kukabiliana na mpanda farasi wa wakati huo, alikuwa ni Mwenye Uhai aliyekuwa na uso wa mwanadamu. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Ule wakati wa watu walioelimika, wale watengenezaji, akina Luther, Wesley, Calvin, Knox, Finney, Moody. Unaona?

139 Lakini basi angalia, ni kitu gani kilichotokea wakati wa jioni? [Ndugu fulani anasema, "Tai!"—Mh.] Tai, unabii unarudi tena. Kutakuwako Nuru wakati wa tai, njia ya Utukufuni hakika mtaiona, Enyi Kanisa la Mungu aliye hai!

140 Laiti ningeweza kuja hapa na—na kuketi tu chini asubuhi moja, na kukaa siku nzima, nifanye ushirika pamoja nanyi kwenye mambo haya. Sikilizeni, je! mnafikiri siwapendi? Ninawapenda, ndugu zangu. Ni—ni—ningetaka kwenda kwenye kila madhehebu na kushiri- . . . na—na kumanini tu na kila mmoja wenu. Lakini, mnaona, haiwezekani kabisa tu. Ni vigumu kupata mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu.

141 Ninaingia kisiri kwenye taifa fulani sasa hivi, kwa sababu ya madhehebu, kwa sababu wasingeruhusu huduma ambayo Mungu . . . Niliwajibu kwa barua, nikasema, "Kwa miaka kumi nimejaribu kuja. Nanyi pamoja na ubatizo wenu wa kichaa!"

142 Mmoja wao eti anaamini, "Unapaswa kubatizwa mara tatu; mara moja kwa Baba, na mara moja kwa Mwana, na Roho Mtakatifu; kifudifudi." Mwingine alisema, "La, unapaswa kubatizwa mara tatu kichalichali; mara moja kwa Mwana, mara moja kwa Baba, na Roho Mtakatifu." Na wote wawili wako makosani.

143 Mmoja alisema, "Yeye, unabatizwa kwa mauti Yake, na Yeye aliinama mbele wakati alipokufa. Sisi tunabatizwa

katika mauti yake." Huyo mwingine alisema, "Je! ni nani anayemzika mtu kifudifudi? Unamzika, kichalichali." Upuuzi mtupu, kuwatenganisha watu, inaonyesha kwamba ni wivu. Limetoka kwa Shetani. Si la Mungu.

144 Katikati ya pande zote mbili, Mungu hayuko upande wo wote, bali anaita kutoka pande zote mbili, "Tokenii kwao, mkatengwe nao," asema Mungu, "nami nitawakaribisha Kwangu." Mungu awabariki.

*Ile Mbegu Haitarithi Pamoja na Kapi* SWA65-0429B
(The Seed Shall Not Be Heir With The Shuck)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi asubuhi, 29 Aprili, 1965, katika Biltmore Hotel kule Los Angeles, California, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org